

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**



TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MADAKTARI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais - TAMISEMI) imepata kibali cha ajira ya Madaktari 610 watakaofanya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Hivyo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inapenda kuwatangazia Madaktari wa Binadamu na Meno waliohitimu katika vyuo mbalimbali vya Elimu ya Juu vinavyotambulika na Serikali kuwasilisha maombi ya nafasi za ajira kuanzia **leo tarehe 24/03/2020** ili kujaza nafasi mbalimbali katika Hospitali za Halmashauri na Vituo vya Afya kama ifuatavyo:-

1. Daktari Daraja la II/Daktari wa Meno Daraja la II (Nafasi 610)

Waombaji wawe na Shahada ya Udaktari wa Binadamu/Meno kutoka Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza mafunzo ya kazi kwa vitendo (*Internship*) kwa muda usiopungua mwaka mmoja na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (*Medical Council of Tanganyika*).

SIFA ZA MWOMBADI;

- i. Awe raia wa Tanzania;
- ii. Awe na umri usiozidi miaka 45;
- iii. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea;
- iv. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali au asiwe Mwajiriwa wa Hospitali za Mashirika ya Dini ambaye mshahara wake unalipwa na Serikali;
- v. Asiwe amewahi kuajiriwa Serikalini; na
- vi. Asiwe na check namba.

MAOMBI YOTE YAAMBATISHWE NA NYARAKA ZIFUATAZO:

- i. Barua ya maombi ya kazi ikieleza Mikoa mitatu ambayo mwombaji angependa kupangiwa kufanya kazi katika moja ya Halmashauri zake;
- ii. Nakala ya cheti cha kidato cha nne/sita;
- iii. Nakala za Vyeti vya Taaluma;

- iv. Nakala ya cheti cha kuzaliwa;
- v. Nakala ya cheti cha usajili kamili (*Full Registration*) au Leseni ya kufanya kazi ya taaluma husika; na
- vi. Maelezo binafsi (CV), yakionesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani/namba za simu za kiganjani za wadhamini wasiopungua wawili.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE

- i. Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi Halmashauri yoyote watakayopangiwa;
- ii. Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi na mashirika/taasisi zilizoingia ubia na Serikali;
- iii. Waombaji waliosoma nje ya nchi wanatakiwa waambatishe *Equivalent Certificate* kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU); na
- iv. Waombaji watakaotuma/waliotuma maombi yao ya kazi Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hawapaswi kuomba nafasi hizi za kazi zilizotangazwa kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Maombi yote yatumwe kwa njia ya mtandao (*online*) kupitia mfumo wa kielektroniki unaopatikana kupitia anuani ifuatayo: ajira.tamisemi.go.tz.

Maombi yoyote yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kuletwa moja kwa moja Ofisini hayatafanyiwa kazi.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10 Aprili, 2020 saa 9:30 alasiri.

Tangazo hili linapatikana katika tovuti yetu

www.tamisemi.go.tz

Limetolewa na: Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais - TAMISEMI,
Mji wa Serikali – Mtumba,
S.L.P 1923,
41185 DODOMA.

24 Machi, 2020